# Dhima ya Mianzo na Miisho katika Nathari za Kiswahili za Fasihi ya Watoto: Mifano kutoka Riwaya na Hadithi za Kiswahili za Watoto nchini Tanzania

Edith B. Lyimo


## Ikisiri

Fasihi ya watoto hutofautiana na fasihi ya watu wazima katika maudhui, fani, mawanda, walengwa na hata umri. Pamoja na kutofautiana huko, bado dhima ya fasihi inabaki ileile ya kufundisha, kuburudisha, kuonya, kuadibu, kurithisha amali za jamii na kadhalika. Wataalamu mbalimbali wa fasihi wakiwapo waandishi, wahakiki, walimu wanaofundisha madarasa ya fasihi na wengineo, wanafahamu kabisa kuwa kazi za fasihi zinatofautiana kwa muundo na hata mitindo. Hawa wanaongozwa na kaida kadha wa kadha zinazotawala kazi hizo. Nathari ni aina mojawapo ya kazi za fasihi ambazo zina kaida zake zinazoitofautisha na aina nyinginezo kama vile ushairi na tamthiliya. Moja ya kaida zake ni kutumia lugha ya mjazo pamoja na kuwa na sifa ya usimulizi au (uhadithi). Pamoja na sifa hizi kazi zote za nathari huwa na mianzo na miisho ambayo huwa na dhima mbalimbali katika kazi hizo. Makala hii inachunguza mianzo na miisho katika nathari za watoto kwa kutumia Nadharia ya Umuundo. Lengo kuu la makala ni kubainisha mianzo na miisho ya nathari za Kiswahili za watoto pamoja na dhima zake.


## 1.0 Utangulizi

Vitu vyote vyenye uhai vimekuwa vikielezwa na kufahamika kuwa vina mianzo na miisho. Vitu vingine visivyo na uhai, vingine vinaweza kuelezeka mianzo yake kutokana na hadithi mbalimbali au pia tafiti mbalimbali ijapokuwa miisho yake ni vigumu kuieleza. Katika lugha ya Kiswahili na lugha nyingine kuna msemo usemao kuwa 'Kila lenye mwanzo halikosi kuwa na mwisho'. Hii ina maana kuwa, haiwezekani kwa kazi fulani ikawa na mwanzo na kukosa mwisho. Hii ni dhahiri kuwa vipengele hivi hutegemeana na kukamilishana. Kwa kuchukua msemo huu katika uwanja wa fasihi tunaweza kudai kuwa kazi yoyote ile ya fasihi, iwe andishi au simulizi ina mahali inapoanzia na inapoishia. Mianzo na miisho hiyo hubeba simulizi mbalimbali nyingine zikiwa na dhima mbalimbali kijamii. Wakitumia mfano wa fasihi wataalamu mbalimbali wanatanabahisha kuwa mianzo na miisho ina dhima maalumu katika kazi husika hivyo isichukuliwe kijuujuu tu.

Akizungumzia kuhusu fasihi simulizi, Senkoro (2006) anasema kuwa kuna ugumu wa kueleza muundo katika tanzu za fasihi simulizi kwa sababu ya kuingiliana kwao. Anaona kuwa urahisi upo katika vitendawili kwa sababu mianzo na miisho yake ni rahisi kuibaini kutokana na kwamba ni ya kifomula. Pamoja na kwamba Senkoro hakuzungumzia kuhusu mianzo na miisho katika fasihi andishi, haina maana kuwa kazi zake hazina mianzo na miisho.

Hood (2012) katika makala yake kuhusu mianzo na miisho ya riwaya anasema kuwa sentensi muhimu kuliko zote mara nyingi ni sentensi ya kwanza kwa sababu ni kama ndoana au mwongozo. Hii ndiyo inayoweza kumteka msomaji. Kama haitaweza kumteka msomaji aweze kuendelea kusoma sentensi

inayofuata basi kazi yako nzima haitakuwa na uhai. Hii ina maana kuwa mwanzo mzuri una maana sana katika kazi ya fasihi. Mwanzo lazima umshawishi msomaji ili aweze kuendelea kusoma sehemu zinazofuata na hatimaye kazi nzima. Akizungumzia umuhimu wa miisho, Hood anasema kuwa msanii baada ya kuandika kazi yake ya ubunifu hana budi kuimalizia. Anasisitiza kuhusu kumaliza kazi kwa kishindo. Lengo la msanii kumaliza kwa kishindo ni ili aweze kukidhi matarajio ya wasomaji wake. Anafananisha mwisho legelege na sinema ambayo imeishia vibaya bila kumaliza kiu ya wasomaji. Maelezo anayotoa Hood yanamaanisha kuwa mianzo na miisho ya kazi za kibunifu ina dhima kubwa katika kazi hizo. Adamo (1995) katika kueleza nguvu ya miisho anasema kuwa mwisho ni kama lakiri ya kufunga kile kilichokuwa kikiendelea. Hapa inamaanisha kuwa mwisho humfanya msomaji afikie mwisho wa hadithi pamoja na kupata kile kilichokusudiwa na mtunzi. Aidha, mwisho humfanya msomaji baada ya kufuata mkondo mwingine wa simulizi wakati ilipoanza hiyo simulizi, aweze kurudi kwenye maisha au mkondo wake wa kawaida. Kwa ujumla wataalamu hawa wa fasihi, wameeleza umuhimu wa mianzo na miisho ya kazi za kifasihi na kusisitiza kwamba isichukuliwe kijuujuu tu kwani ina dhima muhimu katika kazi husika. Makala hii inachunguza mianzo na miisho ya nathari za Kiswahili za watoto ili kubaini dhima ya mianzo na miisho hiyo katika nathari hizo.

Nathari ni moja kati ya makundi mawili makubwa ya fasihi andishi jinginelo likiwa ni nudhumu. Wataalamu wa fasihi (Mulokozi, 1996; Wamitila, 2008, kwa kutaja wachache), wanaeleza kazi ya kinathari kuwa hutumia lugha ya mjazo au ya kawaida katika kufikisha ujumbe. Aidha, ni kazi ambayo kifani inatofautiana na ushairi hasa katika vipendele vya muundo na mtindo. Mathalani, Mulokozi (1996) anasema kuwa nathari ni maandishi ya kimjazo yasiyofuata kanuni za kishairi. Hii ina maana kuwa nathari kimuundo haizingatii beti, au mapigo ya kimuziki. Mulokozi anaendelea kutaja tanzu zilizoko katika nathari kuwa ni pamoja na tamthiliya, hadithi kwa maana ya riwaya, visa, na baadhi ya wasifu na tawasifu. Songoi na Masele (hakuna mwaka) wanabainisha riwaya, novela, romansi na hadithi fupi kama mifano ya nathari. Pamoja na kwamba wataalamu hawa wanatofautiana kidogo katika kubainisha mifano ya nathari, wote wanabainisha sifa kuu ya nathari kuwa lazima iwe katika masimulizi ya kimjazo. Kwa ujumla nathari ina umbo au muundo unaoitofautisha na kazi ya kishairi kama vile kutokutumia sana lugha ya mkato au lugha yenye mapigo ya kimuziki. Ili kukidhi malengo ya utafiti huu, makala inafasili nathari za watoto kama kazi ambazo zimejikita katika masimulizi na zenye kutumia lugha rahisi ya mjazo na ambazo hadhira yake ni watoto. Makala hii pia inafasili dhana ya mtoto kuwa ni mtu mwenye umri wa chini ya miaka kumi na minane, fasili ambayo inatumiwa na Shirika la Kazi Duniani na kwenye Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977. Makala imemakinikia riwaya na hadithi fupi za watoto yaani zilizoandikwa kwa kuwalenga watoto kama hadhira na imeongozwa na Nadharia ya Umuundo kama ilivyofafanuliwa na Warner (2015) katika kubainisha aina

mbalimbali za mianzo na miisho katika vitabu teule vya fasihi ya watoto pamoja na dhima yake. Mpangilio wa makala ni kama ifuatavyo: Sehemu ya kwanza ni utangulizi unaofafanua vipengele vikuu vya makala hii ambavyo ni mianzo, miisho na nathari. Sehemu ya pili ni nadharia iliyoongoza ukusanyaji na uchambuzi wa data kutoka katika vitabu teule. Sehemu ya tatu ni uwasilishaji wa data za mianzo na miisho kutoka vitabu teule. Sehemu ya nne inaonesha dhima ya mianzo na miisho na sehemu ya tano ni hitimisho.

## 2.0 Nadharia ya Umuundo

Makala hii imeongozwa na Nadharia ya Umuundo. Nadharia hii ilianzishwa na mwanaisimu Ferdinand de Saussure. Baadaye Nadharia ya Umuundo ilipata wafuasi na matumizi mengi katika nyanja nyingi. Waasisi wengine wanaohusishwa na Nadharia ya Umuundo ni pamoja na mwanaanthropolojia Claude Levi-Strauss, mwanahistoria Michel Faucault, mwanasayansi ya siasa Louis Althusser, mwanasaikolojia changanuzi Jacques Lacan na mwanafasihi Vladmir Propp.

Kuwezekana kwake kutumika katika nyanja anuwai kunatokana na msingi mkuu wa nadharia hii kwamba, kitu chochote, hata kama kinaonekana kama umbo moja, ni muunganiko wa visehemu mbalimbali. Mathalani, katika karne ya 20 wanaisimu kama vile Ferdinand de Saussure wameitumia sana Nadharia ya Umuundo katika kuelezea muundo wa lugha. de Saussure alifafanua miundo miwili ya lugha ambayo ni umilisi na utendaji. Akihusisha matini, mtaalamu huyu anasema kuwa muundo wa matini upo katika utendaji kwa sababu ni muundo wa lugha katika ujumla wake; na kwa mantiki hiyo kazi ya kifasihi huhusisha lugha ya aina yake. Mwanafasihi Vladmir Propp anaangalia zaidi muundo katika kazi za kifasihi. Mathalani, akitumia hadithi kama kazi ya fasihi Vladmir Propp anasema kuwa hadithi zina vipengele vikuu ambavyo kwa pamoja vinaungana katika kuunda maana moja katika muundo.

Akitofautisha muundo wa kifasihi na wa kiisimu, Xiaohe (1997) kama anavyonukuliwa na Liu (2009) anasema kuwa muundo wa matini ya kifasihi (kama vile riwaya na hadithi) huhusisha zaidi sifa za nje za matini hiyo. Hii ina maana kuwa sifa za nje za matini za kifasihi ndizo zinazotumika katika uchambuzi na siyo sifa za ndani au umilisi. Hata hivyo, Xiaohe (1997) kwa mujibu wa Liu (2009) anasema kuwa muundo wa matini ya kifasihi wakati mwingine ni sawa na muundo wa sayansi asilia kwa sababu hujengwa wakati wa mchakato wa usomaji. Mawazo haya yanamaanisha kuwa muundo wa kifasihi hubainishwa wakati wa usomaji. Hii hutokana na ukweli kwamba katika usomaji ndipo msomaji, mathalani hugundua tofauti ya kazi moja au matini moja na nyingine kutokana na vipengele au matini anazokabiliana nazo, uzoevu alionao pamoja na mtiririko wa kazi husika. Mathalani, kupitia mambo haya atagundua kazi fulani mwanzo wake ni upi na mwisho wake ni upi.

Wafula na Njogu (2007) wanasema kuwa muundo wa fasihi una vipengele vinavyotegemeana na vinavyoelezwa katika muktadha wa vipengele vingine

kutokana na uhusiano wa vipengele hivi kwa pamoja kuikamilisha kazi hiyo. Katika uchambuzi wa kifasihi muundo huchukuliwa kama umbo la nje la kazi au mjengo wa kazi husika (Madumulla, 2009) ambao humwezesha msomaji kujua kuwa huu ni utanzu fulani. Anachokieleza Madumulla ni kwamba muundo ni mwonekano wa kitu kama kilivyo na ambao humwezesha kukitofautisha na kingine. Muundo au umbo hilo hutokana na utungamanisho wa vipengele mbalimbali vinavyoipa sifa kazi hiyo. Liu (2009) anasema kuwa muundo ni kipengele muhimu katika kuchambua kazi za kisanaa ikiwa ni pamoja na kazi za kifasihi kama vile hadithi fupi. Hata hivyo ili kukidhi malengo ya makala hii, Nadharia ya Umuundo katika fasihi kwa mujibu wa Warner (2015) ndiyo iliyotumika kutokana na kuzungumzia vipengele vya kazi ya fasihi kuwa vinakamilishana na kutegemeana. Kwa mujibu wa Warner (2015) muundo ni mjengo unaotokana na vipengele, visehemu au vitu vilivyounganishwa pamoja. Akikazia mawazo haya kwa upande wa fasihi Warner anaeleza kuwa muundo wa fasihi ni kama utungamanisho wa pamoja wa sehemu na vipengele vinavyounda kazi hiyo. Baadhi ya vipengele vya muundo wa kazi ya kifasihi ni mianzo na miisho ambapo tanzu na vipera vyote vya kifasihi zina mianzo na miisho.

Akitoa mfano wa uhusiano wa mianzo na miisho kama vipengele vya kimuundo, Pattison (2012) anasisitiza kuwa mchambuzi wa kazi ya fasihi apitie kazi husika kwa kina ili ahakiki vipengele hivi viwili kuona kama mtunzi amekengeuka mahali fulani au la. Kwa kuzingatia maana na umuhimu wa muundo wa kifasihi kwa mujibu wa wataalamu hawa ni kwamba mianzo na miisho ni kati ya vipengele vya muundo vinavyotegemeana, kuhusiana na kukamilishana. Hii ina maana kuwa vipengele hivi haviwekwi tu kwa bahati mbaya bali kwa lengo au dhima maalumu. Katika makala hii tunabainisha mianzo na miisho katika nathari za watoto na dhima zake kwa kutumia nadharia hii ya Umuundo. Nadharia ya Umuundo imetumiwa kama ifuatavyo: Kwanza kubainisha mwanzo katika kila kazi iliyoteuliwa pamoja na mwisho wake. Kwamba kazi imeanzaje? Na kazi hiyohiyo imeishiaje? Pili, kutokana na mawazo ya Umuundo kwamba vipengele vya kazi fulani ya fasihi hufungamana na kukamilishana (Warner, 2015), nadharia hii imewezesha kubainisha dhima ya mwanzo fulani au mwisho fulani uliobainishwa kwa kuihusisha na vipengele vingine vya kazi husika kama vile wahusika, dhamira, mandhari, na muktadha ambavyo kwa pamoja huunda kazi nzima. Kwa ujumla kazi teule zilichambuliwa kwa kina ili kubaini mianzo na miisho pamoja na dhima zake.

## 3.0 Mbinu na Uchambuzi wa Data

Makala hii ina malengo makuu mawili ambayo ni kubainisha mianzo na miisho ya nathari za watoto kwa kutumia vitabu teule na kueleza dhima ya vipengele hivi katika vitabu husika. Jumla ya vitabu 26 vya Kiswahili vya nathari za watoto viliteuliwa kinasibu ikiwa ni riwaya 16 na hadithi fupi 10. Sababu ya kuteua aina hizi za nathari na kuacha aina nyinginezo za kazi za watoto kama vile tamthiliya

inatokana na ukweli kwamba tamthiliya, tofauti na riwaya na hadithi fupi, huweza kuwa na mianzo ambayo ni maelezo ya jukwaa, ngoma, nyimbo na kadhalika kiasi cha kutobainisha kwa uwazi mwanzo wa simulizi kama ilivyo katika riwaya na hadithi fupi na hivyo kuweza kuathiri hitimisho la jumla la makala yetu. Vitabu hivi vilipatikana katika maktaba binafsi ya mwandishi wa makala hii[1]. Vitabu vyote 26 teule vilisomwa kwa kina ili kuelewa hadithi husika. Kisha vitabu hivyo vilipitiwa tena ili kubainisha mianzo na miisho yake. Mkabala wa ubainishaji ulikuwa kuangalia aya ya kwanza na ya mwisho ya kazi husika. Hatua iliyofuata ilikuwa ni kuhusisha mwanzo au mwisho huo na hadithi nzima. Sehemu inayofuata inabainisha mianzo na miisho iliyobainishwa pamoja na dhima yake katika nathari za Kiswahili za watoto.

## 4.0 Mianzo na Miisho katika Vitabu Teule

Mianzo na miisho kadhaa imebainishwa katika kazi teule. Kwa kuwa hakuna kazi isiyokuwa na mwanzo wala mwisho, jumla ya mianzo 26 na miisho 26 imebainishwa kutoka katika vitabu 26 kama inavyoonekana hapa chini:

| **Mianzo** | **Miisho** |
|---|---|
| (a) MIMI naitwa Mugoya Mahanzala. Nilizaliwa katika kijiji cha Igumbilo, ambacho kiko kilometa kama saba tu kutoka katika mji wa sasa wa Iringa, kwenye njia kuu iendayo Dar es Salaam. Siku niliyozaliwa siifahamu, ila najua kuwa ulikuwa ni wakati wa vita vya Ilundamatwe vya mwaka 1880 kati ya Mutwa Mukwava na mpinzani wake Mwamubambe (*Ngome ya Mianzi*, 2006:1). | (a) Yaliyonipata mimi na Nyawelu na mdogo wetu mchanga katika mapambano ni mengi. Sithubutu kuyasimulia yote leo, kwani mimi nimechoka. Bali siku moja, kama Mungu ataniweka hai, nitayaeleza yote kwenu ili kuwaondolea dukuduku lenu. Kwa leo haya yanatosha, maana wazee walisema, “Asemaye yote husifiwa na wachache.” Hivyo nawaaga nikisema, kama sisi Wahehe tusemavyo, *Twiwonoga, sa yitang’asa lusiku* – Kwa herini ya kuonana (*Ngome ya Mianzi* 2006:49). |
| (b) Hapo zamani za kale katika nchi moja palitokea bwana mmoja aliyeitwa Jojo. Yeye aliishi na mkewe. Maisha yao yalikuwa mazuri kwani hawakuwa na shida. Walikuwa wakulima stadi wa kazi (*Bahati na Mumewe*, 1995: 1) | (b) Bahati na Sina-Kitu wakawa wameponea chupuchupu. Iliwachukua siku tatu kufika makwao. Walipofika, kwanza Baba na Mama Bahati walishangaa sana kuwaona mapema hivyo, wakiwa wenyewe bila Tetemeko, mumewe Bahati. Waliposimuliwa visa vilivyotokea, walimshukuru sana Sina-Kitu kwa ushujaa wake. Walimuasa Bahati kuhusu wageni wasiofahamika. Bahati aliahidi hatarudia kuwa mjinga tena (*Bahati na Mumewe*, 1995: 31) |

[1] Mwandishi wa makala hii amefanya utafiti kuhusu Fasihi ya Watoto katika ngazi ya Uzamivu hivyo ana vitabu vingi vya watoto katika maktaba yake binafsi.

| | |
|---|---|
| (c) Katika nchi ya Zabibu na Asali aliishi msichana mmoja. Jina lake alikuwa Sinderela. Sinderela alikuwa msichana mwenye sura ya kupendeza. Alikuwa mwembamba na mrefu kiasi. Uso wake ulikuwa wa mviringo na midomo yake ilijaa tabasamu wakati wote. Sinderela aliwaheshimu watu wote (*Sinderela*, 1995:2) | (c) Harusi ya Sinderela na mwana wa mfalme ilifana sana. Maharusi waliishi katika jumba la mfalme kwa furaha. Baadaye mwana wa mfalme alitawazwa kuwa mfalme wa nchi ya Zabibu na Asali badala ya baba yake aliyekuwa mzee. Sinderela naye akawa malkia wa nchi hiyo (*Sinderela*, 1995:30) |
| (d) Siku moja mvulana mgeni jina lake Noa alipangwa kujiunga na darasa la kina Wema. Ngozi yake ilikuwa nyeupe sana. Mboni za macho yake zilikuwa za kibluu. Nywele zake zilikuwa kama mvi. Hata nyusi na kope zake zilikuwa nyeupe. Watoto darasani waliogopa kukaa naye kwenye deski moja (*Wema Amwokoa Noa*, 2009:1) | (d) Wanafunzi walikusanyika kumpongeza Wema kwa ujasiri wake. Wakamnyanyua Wema juujuu wakimshangilia na kurudi naye darasani. Kesho yake asubuhi, watoto walipofika shuleni walikuta chati zenye vielelezo vya daktari kuhusu ualbino zimewekwa kwenye ukuta wa matangazo (*Wema Amwokoa Noa*, 2009:35) |
| (e) Ali alikuwa na tabia ya uvivu na husuda. Aliwaonea husuda marafiki na hata ndugu zake. Hali hii iliwatia hofu sana wazazi wake. Mama yake alimsimulia hadithi ifuatayo ili apate funzo (*Wawindaji Watatu*, 2000: 1) | (e) Ali aliposikia kisa hiki aliogopa sana. Tangu siku ile akaacha tabia ya wivu na husuda. Wazazi wake nao walifurahi sana na watu wote wakawa wanampenda (*Wawindaji Watatu*, 2000: 21) |
| (f) Sara aliolewa na Mpanduji. Baada ya sherehe kubwa, familia hii ilianza maisha katika kijiji cha Igake. "Huu ni wakati wa furaha kubwa," Mpanduji alisema, "Nimepata mke ninayempenda sana." (*Zindera*, 2008:1) | (f) Zindera alitabasamu kwa muda bila kuongea. Sara na Mpanduji walitazamana. Pili alikunywa maji taratibu. "Ajabu, Ajabu!" Mpanduji alisema. Kukawa na shangwe kubwa kwa kujumuika wote pale sebuleni (*Zindera*, 2008:65) |
| (g) Hapo zamani za kale palikuwa na Chatu mmoja. Chatu huyo alikuwa mkubwa na mpole. Wanyama wote walimpenda Chatu. Mara nyingi walicheza pamoja (*Chatu na Mbwa*, 2005*:* 1&2) | (g) Hadi leo Chatu anamtafuta Mbwa ammeze. Ndio maana Mbwa akimwona Chatu hufyata mkia wake na kutoa sauti ya kulia kwa uchungu (*Chatu na Mbwa*, 2005*:* 20) |
| (h) "Kwa nini tuhangaike kutafuta pesa kila siku?" Jimi alimuuliza Pembe. "Mbona kuna njia ya kupata fedha nyingi kwa mara moja!" (*Wateka Nyara*, 2006:1) | (h) Wahalifu walishtakiwa na hatimaye kuhukumiwa kwenda jela miaka saba. Pendo alizawadiwa na watu mbalimbali baada ya tukio hilo (*Wateka Nyara*, 2006:22) |
| (i) Katika nchi ya Kobelo kulikuwa na mkulima mmoja maskini sana aliyeitwa Majuto. Majuto alikuwa na mke aliyeitwa Shida. Wanandoa hao walikuwa | (i) Wali ule uliwatosha kwa siku mbili tu na ilipofika siku ya tatu chakula chote kikachacha. Wakakimwaga jalalani. Wakarejea katika maisha yao ya umaskini |

hawajajaliwa kuzaa mtoto. Hivyo waliishi maisha ya upweke na umaskini mkubwa (*Pete ya Bahati*, 2006:1)

kama mwanzo (*Pete ya Bahati*, 2006:26)

(j) Katika kijiji cha Nakatinduka aliishi Mzee Ngayomboteka, mkewe Mholeli na binti zake wawili, Nanjeki na Namikoha (*Chifu Mahawanga*, 2006:1)

(j) Ghafla lile joka likageuka na kuwa binadamu aliyevaa taji la uchifu. Harusi kubwa ilifungwa. Wakaishi kwa raha mustarehe (*Chifu Mahawanga*, 2006:14)

(k) SIKU nyingi zilizopita, aliishi mtu mmoja mkarimu, mcheshi na mwenye mali nyingi. Mtu huyo aliitwa Zumya. Zumya alikuwa na zaidi ya mke mmoja na alijaliwa watoto wengi. Watu wote katika jamii yake walimheshimu na kumpenda ("Kilio cha Zumya" *Joka lenye Vichwa Saba*, 2005:68).

(k) Hatimaye, Zumya alizama mwili mzima. Akawaacha watu wakishangaa, wengine wakilia kwa huzuni. Hata leo, Wafipa wana msemo wao, "Ivyakunzi visulila kuno na Zumya kwene wavisile" (Vya dunia havina mwisho ndiyo maana hata Zumya aliviacha) ("Kilio cha Zumya" *Joka lenye Vichwa Saba*, 2005:71)

(l) Hapo zamani za kale katika kijiji cha Kyaro walikuwepo dada wawili. Dada mkubwa aliitwa Kibo na mdogo aliitwa Mawenzi (*Kibo na Mawenzi*, 2003:2)

(l) Ndio maana hadi leo Mawenzi anaonekana amepasuka na Kibo anaonekana kuwa na kofia nyeupe kichwani kwake (*Kibo na Mawenzi*, 2003:21)

(m) Unataka kupata picha fupi ya maisha ya mtoto Upendo? Alionesha kuwa mchangamfu na mwenye udadisi tangu akiwa mdogo sana. Upendo alitambaa haraka, alitembea haraka na alizungumza mapema (*Ndoto ya Upendo*, 2001:1)

(m) "Siri ya nguvu ni ushindi. Siri ya ushindi ni amani" Upendo alifurahi, alirukaruka, aliimba:

Herufi nzuri
kama maua
Namba nzuri
Kama nyota
Nipe siri uliyompa kaka

Mama yake alikuwa anamngojea (*Ndoto ya Upendo*, 2001:33)

(n) Laba alikuwa msichana mwenye kimo cha wastani. Siha yake ilikuwa nzuri na rangi yake maji ya kunde. Alikuwa na umri wa miaka kumi na sita, akisoma darasa la sita katika Shule ya Msingi kijijini mwao, Baghari (*Laba Msichana Shujaa*, 1999:1)

(n) Jumamosi iliyofuata mzee Delo alikwenda Babati kununua zawadi. Alirudi na cherehani na baiskeli. Pia alikuwa na vitenge kwa ajili ya mama, Aboo na Laba. Garu alipewa shati na kaptula mpya. Familia ilifurahi sana. Wakaahidi kuongeza jitihada katika kilimo na ufugaji (*Laba Msichana Shujaa*, 1999:42)

(o) Wakazi wa Kideli waliendelea kuongelea ujasiri wa Mfalme Famba katika safari ya Mji wa Mawe. Walikuwa bado na majonzi juu ya Sado aliyetoweka wakati wa safari hiyo (*Mji wa Mawe 2*, 1996:1)

(o) Kelele za watu ziliziba masikio, "Sawaa!" Hapo watu hawakuzuilika tena. Waliinuka kuwabeba juu mashujaa wa Kideli. "Famba! Sado! Zumba!" Wakaimba huku wakiwazungusha pale uwanjani. Nuru mpya ya matumaini, usalama na amani iliangaza nchi nzima ya Kideli (*Mji wa Mawe 2*,

| | |
|---|---|
| | 1996:34) |
| (p) Siku niliyoonana na Ndosi uso kwa uso jua lilikuwa kali. Hivyo ilinibidi nipime kwa makini kivuli changu ili kujua kama muda wa kwenda shule tayari. Kivuli changu kilinieleza kuwa muda ulikuwa tayari, maana urefu wa kivuli ulikuwa umepungua. Ulionyesha kuwa saa sita ilikuwa si mbali sana (*Tanzua*, 1991:1) | (p) Nilikaa chini, mwili ukashikwa ganzi. Sikutaka kuyaamini yale maneno. Ndosi amekwishakufa. Nilitamani kulia lakini macho yangu yalikataa kabisa kutoa machozi (*Tanzua*, 1991:54) |
| (q) KUKAMATWA kwa Kangu Mramba kwa tuhuma za kujihusisha na biashara haramu ya madawa ya kulevya, ilikuwa habari kubwa sana (*Mpishi Mwenye Kibiongo*, 2000:1) | (q) Inspekta Mwanana alizungusha kichwa katika hali ya kukata tamaa, akampa Abdul gazeti hilo bila kulisoma. Kisha alitoka nje taratibu, huku akiwa amejiinamia (*Mpishi Mwenye Kibiongo*, 2000:55) |
| (r) Felisia na Hamiata ni marafiki wakubwa. Walianza kuwa marafiki tangu walipokuwa darasa la tano. Hadi sasa wanapomaliza darasa la saba bado ni marafiki (*Mwendo*, 1998:3) | (r) Aaa, sema vizuri we mtoto. Homa imepanda? Felisia alisema akiwa anamkonyeza rafiki yake. Walicheka na kuagana, Hamiata akisema, “nenda zako wee.” Kila mmoja alikwenda njia yake, wote wakiwa na sura zilizojaa mawazo. Felisia aliwaza mambo yake na Hamiata yake (*Mwendo*, 1998:70) |
| (s) Mji wa London ulimsisimua sana Helena. Toka walipotua katika uwanja maarufu wa Heathrow hadi wanapanda treni kuelekea mjini, macho ya mshangao yalikuwa yamemtoka (*Vipaji vya Helena*, 2009:1) | (s) Helena alizidi kuchanganyikiwa. Alipoteza sauti. Kwa uso uliolowa machozi aliwatazama mama na baba yake wa kufikia katika hali ya kuwashawishi wamsaidie. Bw. Macbain alijawa na tabasamu pana lililomfanya aonekane kijana zaidi. Bibi Macbain alikuwa akifuta machozi. Helena akaangua kilio (*Vipaji vya Helena*, 2009:47) |
| (t) Kando ya mto Lumemo kulikuwa na mti mkubwa wa Mkuyu. Katika mti huo waliishi Ngedere wengi, wakubwa na wadogo. Pia katika mti huohuo kulikuwa na mamba wengi, wakubwa na wadogo (*Urafiki wa Ngedere na Mamba*, 2008:1) | (t) Mamba mdogo aliogelea kwa kasi hadi wakafika eneo ambalo wanachezea. Hapo Ngedere mdogo akachupa kutoka mgongoni mwa mamba na kurukia mti mkubwa wa mkuyu. Alipofika kileleni mwa mti Ngedere Mdogo alisema, “Wajinga ndio waliwao”. Mamba mdogo akasema, “Si mimi, ni wazazi wangu walionishawishi”. Ngedere hakurudi (*Urafiki wa Ngedere na Mamba*, 2008:16) |
| (u) Mwenzangu mpendwa, mimi nimepungua nini? Nikinyosha mkono wangu haufiki kwako. Nikipiga mayowe hunisikii. Nikikodoa macho yangu sikuoni. Lakini mimi najua kuwa wewe upo hapo. | (u) Nilikuwa nikisikia maumivu makali mno yakitokea sehemu ya chini ya tumbo langu. Nilishikwa mkono kurudishwa nyumbani. Kila hatua niliyoipiga ilinitonesha kwenye jeraha. Sikujua kama ule ndio mwisho wa huo |

Ningependa kukueleza yaliyomo moyoni mwangu. Ningependa nawe unieleze yako (*Sababu Mimi ni Mwanamke*!, 1999:1-2).

(v) Chausiku alisoma darasa la sita wakati Masharubu, mtu mzima, alipoanza kumshawishi awe mpenzi wake. Msichana huyo alikuwa haelewi mambo ya mapenzi zaidi ya kusikia au kusoma gazetini. Chausiku aliishi na wazazi wake mjini Tanga. Njia yake ya kuendea shule ilipita katika kituo cha teksi ambapo Masharubu, aliyekuwa dereva, alimwona kwa mara ya kwanza (*Mtego Kabambe*, 2003:1)

(w) Helena!...Haraka njoo nyumbani!" sauti ya mama iliniita. Ilikuwa sauti kali nzito, iliyojaa hofu na mashaka. Huko nyuma sikupata kuisikia sauti ya mama kuwa namna hiyo (*Kimbia! Helena, Kimbia!*, 2005:1)

(x) "NILIDHANI ulisema kuwa mimi nimekuwa mwanao! Nilidhani utanilea hadi ukubwani, ili nami nikulee uzeeni!" Helena aliirudia tena kauli aliyokuwa ameitoa muda mfupi uliopita. Kauli ambayo ilikuwa imemchoma sana mzee John Murego na kumfanya atokwe na machozi (*Cheka Kidogo, Helena!*, 2007:1)

(y) Mishale ya saa ilionyesha saa 12:30 asubuhi. Anga la mashariki halikuwa samawati tena. Miali ya jua, nyuma ya Mlima Meru, ililifanya anga kuwa njano. Wakati huu mji wa Arusha ulizizima kwa baridi kali. Daudi alikurupuka kitandani upesi, akidhani amechelewa shuleni (*Polisi Kipofu*, 2003:1)

(z) Wakati wa enzi za usultani na ufalme, kulikuwa na nchi moja iliyoitwa Mkira. Katika nchi hiyo aliishi mtu mmoja aliyeitwa Pazi. Pazi alikuwa fukara sana. Lakini hakuridhika na hali hiyo. Alitafuta njia ya kupata mali (*Mganga Pazi*, 2003:2)

mkasa wa lile balaa, au kitu gani kitafuata. Nilikuwa ni hoi lakini bado ni hai (*Sababu Mimi ni Mwanamke*!, 1999:38).

(v) Ukweli kuwa Chausiku angeambukizwa UKIMWI, ulidhihirika. Baada ya kufungwa jela, Masharubu alifariki dunia kwa UKIMWI. Kutokana na tukio hilo, hadi leo Chausiku anauogopa UKIMWI na amebadili kabisa tabia yake. Lakini msisimko wa tukio hilo bado haujasahaulika hata leo (*Mtego Kabambe*, 2003:27)

(w) Muda mfupi baadaye tulikuwa ndani ya basi liitwalo daladala, tukielekea Upanga, tulikoelekezwa kuwa ndiko ziliko ofisi za Umoja wa Mataifa (*Kimbia! Helena, Kimbia!*, 2005:56)

(x) Waliyoyoma zaidi angani. Punde Helena hakuweza kuona chochote tena ardhini. Akahamisha macho yake kutazama mawingu ambayo pia rubani aliyaacha chini na kupaa juu zaidi! Kwa kheri Dar es Salaam, kwa kheri Tanzania, aliwaza (*Cheka Kidogo, Helena!*, 2007:58)

(y) Daudi atafakari yote aliyoelezwa. Hakufikia kilele cha usanii bila jitihada. Sasa alijiamini kuliko wakati wowote uliopita, katika maisha yake! Kumbe wasiwasi na kutojiamini ni ugonjwa tosha (*Polisi Kipofu*, 2003:54)

(z) Sifa hizi zilizidi kuenea naye Pazi akazidi kujipatia utajiri mkubwa. Lakini moyoni alijua ujanja wake ulikuwa karibu kugundulika. Hivyo siku moja, kwa siri sana, yeye na mkewe walikusanya vitu vyao vyote, haoo, wakatoroka (*Mganga Pazi*, 2003:36).

**4.1 Dhima ya Mianzo katika Nathari za Kiswahili za Watoto**

Katika uchambuzi uliofanyika, tumepata mianzo mbalimbali. Mianzo hiyo inatofautiana baina ya kazi moja na nyingine. Hivyo ina dhima mbalimbali katika kazi hizo za kinathari za watoto kama ifuatavyo:

a) *Kubainisha Majina ya Wahusika*

Katika kazi teule ipo mianzo iliyoanza kwa majina ya wahusika wa hadithi au riwaya husika. Kazi hizo zina majina ya wahusika kama: Felista na Hamiata ni marafiki… (*Mwendo,* 1998:1); Laba alikuwa msichana… (*Laba Msichana Shujaa* 1999:1); Chausiku alisoma….wakati Masharubu… (*Mtego Kabambe*, 2003:1); Helena! Njoo haraka… (*Kimbia! Helena, Kimbia!*, 2005:1); Sara aliolewa na Mpanduji… (*Zindera*, 2008:1) kwa kubainisha mifano michache. Kwa kuchunguza mianzo hii tumegundua kuwa majina hayo yanahusiana na hadithi husika; yaani majina ya wahusika wa hadithi teule. Wahusika wa kifasihi huweza kuwa viumbe vyenye uhai (watu, wanyama wengine na mimea) na hata viumbe visivyo na uhai. Kwa ujumla wahusika ndio hutenda, hutendwa, hutendewa, hutendeana, au kutendana matendo mbalimbali.

Tumegundua kwamba majina haya yametokea tangu mwanzo hadi mwisho wa hadithi na ni majina ya pekee. Aidha, majina haya yalikwa ya binadamu, na yalitajwa na msimulizi wa hadithi au mhusika mwenyewe kujitaja au kutajwa na nafsi nyingine. Ni majina ya wahusika wakuu wa hadithi hizo. Hivyo dhima ya mianzo hii ni kudokeza wahusika wakuu wa hadithi. Ilibainika pia kuwa kulikuwa na udokezaji wa wahusika wakuu katika miktadha tofauti ya mianzo. Katika vitabu teule vya riwaya majina haya ya wahusika wakuu yalikuwa mwanzoni au katikati katika sentensi ya kwanza kabisa huku katika hadithi fupi (ngano) majina haya yalikuwa mwishoni mwa sentensi. Mpangilio huu kwa upande wa hadithi fupi za kingano umetokana na kaida yake ya kuwa na mianzo ya kifomula tofauti na riwaya ambazo mianzo maalum ya kifomula si nduni yake bainifu.

b) *Kujenga Taharuki*

Dhima nyingine ya baadhi ya mianzo ni kujenga taharuki kwa wasomaji. Mathalani, katika *Kimbia! Helena, Kimbia!* tunaona jinsi mwandishi anavyojenga taharuki - kwamba mama anamwita Helena arudi nyumbani haraka huku sauti yake ikiwa tofauti. Kwa kutumia mtindo huu, msomaji anapata shauku ya kutaka kujua sababu za mama kuita kwa sauti hizo tofautitofauti. Aina na uzito wa taharuki hutegemea jinsi mwandishi anavyoamua. Kwa mfano, kukamatwa kwa Kangu Mramba kwa tuhuma za kujihusisha na biashara haramu ya madawa ya kulevya, ilikuwa habari kubwa sana (*Mpishi Mwenye Kibiongo*, 2000: 1). Katika mfano huu, mwandishi anaanza kwa kueleza hatma ya hadithi ya *Mpishi Mwenye Kibiongo* kwamba mhusika mkuu wa dawa za kulevya, ambaye ni Kangu Mramba amekamatwa. Kitendo ambacho kilipaswa kuonekana mwishoni ndicho kinachoanza. Taharuki hii imejengwa kwa mbinu ya kiurejeshi wa kimasimulizi.

Kwa kawaida kazi nyingi za watoto hutumia mbinu ya moja kwa moja kama moja ya nduni zake (Lyimo, 2014). Halikadhalika, msomaji anajenga taharuki ya kutaka kujua hofu ya mama imesababishwa na nini? Kwa ujumla kupitia mifano hii tunaona kuwa dhima ya mianzo kama hii ni kujenga udadisi na taharuki kwa wasomaji wa kufuatilia kisa kutokana na kutaka kujua ilikuwaje mpaka mtuhumiwa akakamatwa. Taharuki ni kichocheo kinachomfanya msomaji aendelee kufuatilia kisa au hadithi husika.

c) *Kubainisha Mahali au Eneo la Tukio*

Imebainika pia kuwa ipo pia mianzo yenye dhima ya kubainisha mahali au eneo ambalo kisa kimetendekea au kuibuliwa. Kwa mfano, nchi ya Kobelo alikoishi mkulima maskini sana anayeitwa Majuto… (*Pete ya Bahati*, 2006:1); kando ya mto Lumemo ulipokuwapo mti mkubwa wa Mkuyu walipoishi ngedere wengi, wakubwa na wadogo na ndani ya mto mamba wengi, wakubwa na wadogo (*Urafiki wa Ngedere na Mamba*, 2008:1); kijiji cha Nakatinduka alipoishi Mzee Ngayomboteka (*Chifu Mahawanga*, 2006:1); mji wa London ulimsisimua sana Helena (*Vipaji vya Helena*, 2009:1) na maeneo mengineyo. Maeneo haya yametumiwa na waandishi katika kuumba mandhari pamoja na aina ya wahusika, tajiriba zao na masuala mengine ambayo yamewezesha kazi husika kuwa na uhalisi au kukidhi matakwa ya watunzi. Mifano hii tukiihusisha na hadithi husika tunaona kuwa inahusu eneo ambalo ama mhusika mkuu anatokea, au chanzo cha mgogoro, au eneo la matukio muhimu. Hivyo dhima ya mianzo yenye kutaja maeneo au mahali ni kuonesha sehemu ambazo wahusika wakuu wanatokea au maeneo ambayo matukio yanatendekea. Maeneo haya mengine ni dhahania na mengine ni halisi.

d) *Kubainisha Muda, Kipindi cha Tukio Kuanza au Kutokea*

Makala hii pia imebaini kuwa ipo mianzo mbayo hutumiwa na mwandishi ili kubainisha muda au kipindi ambacho kisa kilianza. Mathalani, mwandishi anasema "Mishale ya saa ilionyesha saa 12:30 asubuhi. Anga la mashariki halikuwa samawati tena. Wakati huu mji wa Arusha ulizizima kwa baridi kali. Daudi alikurupuka kitandani upesi, akidhani amechelewa shuleni" (*Polisi Kipofu*, 2003:1). Mfano huu unaonesha muda wa kuanza kwa tukio au kisa; kisa kimeanza kupata mwanzo kipindi cha asubuhi. Kila muda anaoutumia mtunzi huwa na athari katika hadithi husika. Mathalani, muda wa asubuhi huwa una mambo na taarifa nyingi mpya kuliko muda wa jioni. Hii hutokana na kujumuisha taarifa na matukio ya usiku ambapo watu huyapata mara nyingi kwa wakati mmoja kutokana na kushindwa kuyapata yote wanapokuwa usingizini au wamesinzia tofauti na mchana ambapo watu huweza kupata taarifa na matukio mbalimbali kwa muda tofautitofauti. Aidha wakati wa asubuhi mara nyingi watu wanakuwa hawajachoka na akili zao huruhusu kupokea mambo vizuri kuliko muda wa jioni au mchana ambapo watu wengi huanza kuchoka kutokana na kazi mbalimbali. Hivyo muda ni

muhimu sana katika utunzi wa kazi za fasihi. Muda hubeba taarifa ambazo husaidia katika kujenga kisa na migogoro mbalimbali. Asubuhi ni muda ambao akili za watu wengi zimetulia na mtu anaweza kusikiliza jambo analoambiwa kwa umakini mkubwa ikilinganishwa na muda mwingine.

e) *Kumtambulisha Msimulizi*

Kumtambulisha msimulizi ni dhima nyingine ambayo imejitokeza kupitia mianzo ya vitabu teule. Kwa mfano: "Mimi naitwa Mugoya Mahanzala. Nilizaliwa katika kijiji cha Igumbilo, ambacho kiko kilometa kama saba tu kutoka katika mji wa sasa wa Iringa, kwenye njia kuu iendayo Dar es Salaam" (*Ngome ya Mianzi*, 2006:1). "Helena!... Haraka njoo nyumbani!" Sauti ya mama iliniita (*Kimbia! Helena, Kimbia!*, 2005:1), na "NILIDHANI ulisema kuwa mimi nimekuwa mwanao! Nilidhani utanilea hadi ukubwani, ili nami nikulee uzeeni!" Helena aliirudia tena kauli aliyokuwa ameitoa muda mfupi uliopita. Kauli ambayo ilikuwa imemchoma sana mzee John Murego na kumfanya atokwe na machozi (*Cheka Kidogo, Helena!*, 2007:1). Wahusika wanaotajwa katika mifano hii mbali na kuwa ni wahusika wakuu, pia ndio waliowasilisha kisa kwa hadhira. Hivyo dhima ya mianzo hii ni kutambulisha msimuliaji wa hadithi husika.

f) *Kubainisha Chanzo cha Mgogoro*

Kazi nyingi za fasihi hasa riwaya huwa na migogoro - pale ambapo pande mbili au zaidi zinapotofautiana. Mgogoro unaweza kuwa wa nafsi au baina ya mtu na mtu na kadhalika. Migogoro huwa na vyanzo tofauti na vyenye athari mbalimbali katika kazi hiyo. Mathalani, "Kwa nini tuhangaike kutafuta pesa kila siku?" Jimi alimuuliza Pembe. "Mbona kuna njia ya kupata fedha nyingi kwa mara moja!" (*Wateka Nyara*, 2006:1). "Mwenzangu mpendwa, mimi nimepungua nini? Nikinyosha mkono wangu haufiki kwako. Nikipiga mayowe hunisikii. Nikikodoa macho yangu sikuoni. Lakini mimi najua kuwa wewe upo hapo…." (*Sababu mimi ni Mwanamke*!, 1999:1).

Katika jamii kuna mambo kadhaa yanayosababisha matatizo. Mathalani, utekaji nyara ni suala baya na ambalo halipendwi na wanajamii kwa sababu husababisha hofu na vitisho dhidi ya familia au jamii iliyotekwa. Katika mifano hii tunaona mwandishi anaanza kwa kutoa sababu za utekaji nyara kuwa ni ili kupata fedha. Aidha, suala la kupuuzwa au kutokusikilizwa kwa mwanamke nalo limeonekana pia kuwa chanzo cha mtanziko na matatizo mengi anayoyapata mwanamke. Kwa kuchunguza mianzo hii tunaona kuwa dhima yake ni kudokeza chanzo cha mgogoro au chanzo cha kisa husika.

g) *Kurejelea au Kudokeza Jambo/Tukio Lililokwishapita ili kutoa Usuli*

Kupitia data iliyopatikana imebainika pia kuwa mianzo mingine ilikuwa ya kudokeza matukio yaliyopita. Mathalani, Siku niliyoonana na Ndosi uso kwa uso jua lilikuwa kali. Hivyo ilinibidi nipime kwa makini kivuli changu ili kujua kama

muda wa kwenda shule tayari (*Tanzua*, 1991:1). "NILIDHANI ulisema kuwa mimi nimekuwa mwanao! Nilidhani utanilea hadi ukubwani, ili nami nikulee uzeeni". Helena aliirudia tena kauli aliyokuwa ameitoa muda mfupi uliopita (*Cheka Kidogo, Helena!* 2007:1). Katika mifano hii tunaona kuwa mwandishi wa kazi husika anairejesha hadhira kwenye matukio ya nyuma. Msomaji anapokutana nayo mwanzoni hujenga au hupata picha kuwa kuna matukio ambayo yameshapita yanayohusiana na mianzo hiyo. Hivyo dhima ya mianzo kama hii ni kurejelea jambo au tukio lililotangulia au lililokwishapita ili kupata usuli wa jambo linalokusudiwa kuelezwa.

h) *Kudokeza kuhusu Hadithi au Kisa Tangulizi*

Mianzo pia huweza kudokeza kisa kilichotangulia kwa kutumia vipengele vya fani au maudhui kama vile wahusika au mandhari. Mathalani, Wakazi wa Kideli waliendelea kuongelea…Walikuwa bado na majonzi juu ya Sado… (*Mji wa Mawe 2*, 1996:1). Mfano huu unadokeza hali ya kuwapo kwa kisa kingine kabla ya kisa chenyewe kinachokusudiwa. Maneno yaliyotumika kama vile 'Wakazi… waliendelea kusubiri' na 'Walikuwa bado na…' hudokeza kuwapo kwa kazi nyingine tangulizi. Hivyo mianzo kama hii humtaka msomaji kabla ya kuendelea kusoma kazi aliyonayo, asome kwanza kazi iliyotangulia. Hivyo dhima ya mwanzo kama huu ni kumdokezea msomaji kuwa kisa kinachosimuliwa ni mwendelezo wa kisa kingine kilichotangulia.

i) *Kushirikisha Hadhira katika Tafakuri*

Makala hii pia imebaini kuwa baadhi ya waandishi huanza kazi zao kwa kuishirikisha hadhira. Mwandishi anaweza kuanza kwa kutumia lugha ambayo inamfanya msomaji naye awe sehemu ya wahusika. Kwa mfano, "Mwenzangu mpendwa, mimi nimepungua nini? Nikinyosha mkono wangu haufiki kwako. Nikipiga mayowe hunisikii. Nikikodoa macho yangu sikuoni. Lakini mimi najua kuwa wewe upo hapo" (*Sababu mimi ni Mwanamke*!, 1999:1). Mfano huu, mwanzo unaonesha msimuliaji akielekeza simulizi si kwa hadhira tu bali kwa mtu anayefanana naye. Huyu anaweza kuwa binti au mwanamke kama yeye au mwingine yeyote ambaye atakuwa anafanana naye katika hali moja au nyingine au kuwa kwenye mazingira yanayofanana. Dhima ya mwanzo kama huu ni kuifanya hadhira ishiriki na ione kuwa ni sehemu ya yale yanayosimuliwa.

j) *Kubainisha Athari za Fasihi Simulizi katika Fasihi Andishi/ Mwingiliano Matini*

Tafiti na maandiko mengi yanaonesha kuwa kuna uhusiano mkubwa baina ya fasihi andishi na fasihi simulizi-kwamba fasihi andishi huchota vipengele mbalimbali vya kifani kutoka fasihi simulizi. Kupitia kazi teule tumebaini dhima nyingine ya mianzo katika kazi hizo ni kubainisha athari hii ya fasihi simulizi katika fasihi andishi. Kwa mfano, SIKU nyingi zilizopita, aliishi mtu mmoja mkarimu,

mcheshi na mwenye mali nyingi. Mtu huyo aliitwa Zumya. Zumya alikuwa na zaidi ya mke mmoja na alijaliwa watoto wengi (angalia hadithi ya "Kilio cha Zumya" katika *Joka lenye Vichwa Saba*, 2005:68). Pia mfano huu: Siku moja mvulana mgeni jina lake Noa alipangwa kujiunga na darasa la kina Wema (*Wema Amwokoa Noa*, 2009:1). Wataalamu mbalimbali walioshughulikia hadithi fupi au ngano (Mulokozi, 1996, Senkoro, 2011) wanasema kuwa mianzo ya aina iliyobainishwa katika data hii ni ya kawaida kwa ngano, ambacho ni kipera katika fasihi simulizi. Dhima ya mianzo kama hii ni kuonesha athari ya fasihi simulizi katika fasihi andishi. Aidha mianzo hii pia hudokeza dhana ya mwingiliano tanzu/matini katika kazi za fasihi.

**4.2 Dhima ya Miisho katika Nathari za Kiswahili za Fasihi ya Watoto**

Miisho mbalimbali ya nathari za Kiswahili za watoto pia ina dhima anuwai kama ifuatavyo:

a) *Kuonesha Msimulizi wa Hadithi*

Kama ilivyo kwa mianzo, makala hii imebaini pia kuwa baadhi ya miisho inabainisha pia msimulizi wa hadithi, kama inavyoonekana katika dondoo hii:

> Yaliyonipata mimi na Nyawelu na mdogo wetu mchanga katika mapambano ni mengi. Sithubutu kuyasimulia yote leo, kwani mimi nimechoka. Kwa leo haya yanatosha, maana wazee walisema, "Asemaye yote husifiwa na wachache." Hivyo nawaaga nikisema, kama sisi Wahehe tusemavyo, *Twiwonoga, sa yitang'asa lusiku* – Kwa heri ya kuonana (*Ngome ya Mianzi*, 2006:49).

Kwa kutumia mfano huu, tunaona kuwa msimulizi ni wakala wa mwandishi. Anatumia nafsi ya kwanza umoja. Nafsi hii ndiyo iliyoanza kusimulia hadithi ya *Ngome ya Mianzi*. Dhima ya kutumia mwisho huu ni kuonesha msimulizi wa mwisho wa hadithi. Lengo la kutumia nafsi ya kwanza kuanzia mwanzo hadi mwisho ni kuonesha kuwa msimulizi ameshuhudia kila tukio lililotokea na hivyo kumwaminisha msomaji kuhusiana na kile kinachosimuliwa. Pia anadokeza kuwa kutakuwa na mwendelezo wa hadithi hii.

b) *Kubainisha Athari za Fasihi Simulizi katika Fasihi Andishi*

Katika makala hii pia tumebaini kuwa miisho mingine ni ya kifasihi simulizi kama ilivyo kwa baadhi ya mianzo. Kwa mfano, Hatimaye, Zumya alizama mwili mzima. Akawaacha watu wakishangaa, wengine wakilia kwa huzuni. Hata leo, Wafipa wana msemo wao, "Ivyakunzi visulila kuno na Zumya kwene wavisile" (Vya dunia havina mwisho ndiyo maana hata Zumya aliviacha) (Angalia "Kilio cha Zumya" *Joka lenye Vichwa Saba*, 2005:71). Mfano mwingine ni: Ghafla lile joka likageuka na kuwa binadamu aliyevaa taji la uchifu. Harusi kubwa ilifungwa. Wakaishi kwa raha mustarehe (*Chifu Mahawanga*, 2006:14).

Kwa kuchunguza miisho hii tunaona kuwa inafanana na miisho ya visa ambavyo vinapatikana katika fasihi simulizi, hususan katika ngano. Dhima ya kutumia miisho hii ni kuonesha mwingiliano wa fasihi andishi na simulizi. Kwa

mujibu wa Mulokozi (1996), fasihi andishi huchota baadhi ya vipengele vyake kutoka fasihi simulizi. Kwa mujibu wa Wananadharia ya Mwingiliano Matini kuingiliana kwa tanzu au matini ni mbinu inayotumika katika kazi za kifasihi. Akitoa mfano wa kuingiliana kwa kazi za fasihi andishi, hususan hadithi fupi, novela na riwaya, Wamitila (2002) anasema kuwa mwingiliano huo ni wa kawaida kwa sababu kazi hizi hutumia stadi za utunzi zinazofanana. Kwa mantiki hii, mwingiliano wa tanzu katika kazi za kifasihi ni mbinu muhimu katika kutunga kazi hizi. Kutokana na data hii ni wazi kuwa kazi za kinathari za fasihi andishi za watoto hutumia vipengele vya fasihi simulizi kama nguzo kuu ya utunzi.

c) *Kuonesha Funzo/Adili*

Kupitia uchambuzi wa kazi teule tumebaini kuwa baadhi ya miisho hubeba funzo la hadithi au kisa husika. Kuna baadhi ya kazi zilizoonesha miisho yenye dhima hii. Kwa mfano, Wali ule uliwatosha kwa siku mbili tu na ilipofika siku ya tatu chakula chote kikachacha. Wakakimwaga jalalani. Wakarejea katika maisha yao ya umaskini kama mwanzo (*Pete ya Bahati*, 2006:26) na; Jumamosi iliyofuata mzee Delo alikwenda Babati kununua zawadi. Alirudi na cherehani na baiskeli. Pia alikuwa na vitenge kwa ajili ya mama, Aboo na Laba. Garu alipewa shati na kaptula mpya. Familia ilifurahi sana. Wakaahidi kuongeza jitihada katika kilimo na ufugaji (*Laba Msichana Shujaa*, 1999:42).

Kwa kuangalia miisho hii na kuihusisha na mianzo yake tunaona kuwa miisho hii inatoa mafunzo tofauti kwa jamii. Katika jamii aliyoishi Laba na familia yake funzo linalopatikana ni kwamba kufanya kazi za kilimo na ufugaji kuna tija. Katika jamii yenye umaskini juhudi na maarifa vinatakiwa ili kuondokana na hali ya umaskini. Katika jamii ya kina Bahati funzo linalopatikana ni kwamba watu wote si wa kuwaamini.

d) *Kuonesha Mtazamo wa Mwandishi*

Katika uchambuzi wa miisho katika kazi teule, imebainishwa kuwa baadhi ya miisho hii hubeba mtazamo wa mwandishi. Mfano: Kwa leo haya yanatosha, maana wazee walisema, "Asemaye yote husifiwa na wachache." Hivyo nawaaga nikisema, kama sisi Wahehe tusemavyo, *Twiwonoga, saa yitang'asa lusiku* – Kwaheri ya kuonana (*Ngome ya Mianzi*, 2006:49) na "Vya dunia havina mwisho…" katika hadithi ya "Kilio cha Zumya" kitabu cha *Joka lenye Vichwa Saba* (2005:71). Kwa kuchunguza miisho hii tunaona kuwa imetokana na mchujo wa mawazo mengi katika jamii. Ni miisho yenye maneno mazito, ya hekima na pengine mtazamo wa mwandishi.

e) *Kujenga Taharuki*

Kama ilivyo katika mianzo, miisho pia hutumika katika kujenga taharuki. Mwandishi hutumia mwisho ambao licha ya kwamba ameonesha mwisho, mwisho wake haumalizi kiu ya wasomaji; humpa msomaji shauku ya kutaka kujua tukio litakalofuata. Wasomaji hutaka hadithi iendelee. Mfano; "Muda mfupi baadaye tulikuwa ndani ya basi liitwalo daladala, tukielekea Upanga, tulikoelekezwa kuwa

ndiko ziliko ofisi za Umoja wa Mataifa" (*Kimbia! Helena, Kimbia!*, 2005:56). Mwisho kama huu unamwachia msomaji maswali. Msomaji anajiuliza maswali kuhusiana na mhusika Helena. Je, Helena ataambiwa nini huko kwenye ofisi hizo? Je, atasaidiwa? Hivyo miisho kama hii hujenga taharuki ya kutaka kujua hatima ya kile kinachoelezwa.

f) *Kuonesha Suluhisho*

Uchambuzi wa kazi teule za makala hii umeonesha pia kuwa, kuna miisho, hususan katika kazi zilizokuwa na migogoro, inayobeba masuluhisho. Baadhi ya miisho yenye dhima hii ni kama hii: Kelele za watu ziliziba masikio, "Sawaa!" Hapo watu hawakuzuilika tena. Waliinuka kuwabeba juu mashujaa wa Kideli. "Famba! Sado! Zumba!" Wakaimba huku wakiwazungusha pale uwanjani. Nuru mpya ya matumaini, usalama na amani iliangaza nchi nzima ya Kideli (*Mji wa Mawe 2*, 1996:34); Zindera alitabasamu kwa muda bila kuongea. Sara na Mpanduji walitazamana. Pili alikunywa maji taratibu. "Ajabu, Ajabu!" Mpanduji alisema. Kukawa na shangwe kubwa kwa kujumuika wote pale sebuleni (*Zindera*, 2008:65). Pia angalia *Wateka Nyara* (2006:22) na *Wema Amwokoa Noa* (2009:35). Kwa kuchunguza mifano hii tunaona kuwa inaonesha hatma ya kisa/hadithi au mgogoro. Dhima ya miisho hii ni kutoa suluhisho la mgogoro uliojengwa, na hivyo kukidhi haja ya utunzi, mtunzi na msomaji. Aidha, miisho hii pia huonesha mustakabali wa jambo au tatizo lililokuwa linajadiliwa.

g) *Kuonesha Hali Ilivyo Leo*

Dhima nyingine ya miisho iliyobainishwa kupitia uchambuzi wa kazi teule ni kuonesha hali ilivyo leo hii. Mfano, Ndio maana hadi leo Mawenzi anaonekana amepasuka na Kibo anaonekana kuwa na kofia nyeupe kichwani kwake (*Kibo na Mawenzi*, 2003:21), na Ndio maana Mbwa akimwona Chatu hufyata mkia wake na kutoa sauti ya kulia kwa uchungu (*Chatu na Mbwa*, 2005:20). Mifano hii inahusu mazingira au hali ilivyo sasa. Aidha, miisho hii inahusiana na visasili, yaani hadithi zinazoonesha asili ya viti na ambazo zinaambatana na imani za watu. Hivyo dhima ya miisho kama hii ni kuonesha hali ilivyo leo hii katika jamii ijapokuwa mifano hiyo inahusu mikabala tofauti.

h) *Kuipa Hadhira Uhuru wa Kutathmini au Kutoa Hukumu*

Makala hii pia imebaini kuwa baadhi ya miisho ina dhima ya kuipa hadhira uhuru wa kufanya tathmini na kutoa hukumu badala ya kumwachia mwandishi peke yake. Kwa mfano, Doto anainama. Mama amempata. Anakwenda kubadilisha nguo. Lakini atabadilisha utundu? (*Kurwa na Doto. Doto ni yupi*?); walicheka na kuagana. Hamiata akisema "Nenda zako wee." Kila mmoja alikwenda njia yake, wote wakiwa na sura zilizojaa mawazo. Felisia aliwaza mambo yake na Hamiata yake (*Mwendo*, 1998:70), na kisha alitoka nje, taratibu, huku akijiinamia (*Mpishi Mwenye Kibiongo*, 2000:55). Kwa kuchunguza miisho hii tunaona kuwa mwandishi hatoi jibu yeye bali anaiachia hadhira tafakuri. Kwa mujibu wa wataalamu walioshughulikia muundo katika fasihi wanaona kuwa uchambuzi wa

kina wa kipengele fulani hauishii tu kwenye kazi inayochambuliwa, bali pia huhusisha pia matini nyingine alizonazo msomaji wakati wa usomaji (Xiaohe, 1997). Hivyo dhima ya miisho kama hii iliyobainishwa ni kumpa msomaji uhuru wa kutathmini na kuamua kuhusu masuala mbalimbali yaliyojadiliwa katika hadithi.

i) *Kutoa Majibu ya Maswali Yaliyoulizwa*

Katika uchambuzi wa kazi teule imebainika pia kuwa miisho mingine inahusika katika kutoa majibu ya maswali yaliyoulizwa katika kisa au hadithi husika. Mfano "Siri ya nguvu ni ushindi. Siri ya ushindi ni amani" (*Ndoto ya Upendo*, 2001:33). Katika hadithi fupi ya *Ndoto ya Upendo* moja kati ya maswali yaliyoulizwa ni pamoja na kutaka kujua siri ya nguvu ni nini? Baada ya kusoma hadithi yote, hatimaye anatoa jibu mwishoni kabisa. Hivyo dhima ya miisho kama hii ni kutoa majibu ya maswali yaliyoulizwa katika hadithi. Pattison (2012) anashadidia kuwa tatizo litakalozungumziwa mwanzoni katika hadithi, lazima litatuliwe au lipatiwe ufumbuzi katika hadithi hiyo na si jingine. Hii inamaanisha kuwa mianzo na miisho ni vipengele ambavyo vina uhusiano mkubwa sana kwani vinategemeana na kukamilishana katika kuipa kazi maana.

## 5.0 Hitimisho

Makala hii imechunguza na kubainisha mianzo na miisho katika nathari za watoto pamoja na dhima zake. Kwa ujumla nathari za Kiswahili za watoto zina mianzo na miisho yenye dhima anuwai kama vile kubainisha wahusika wakuu, kuonesha eneo la tukio, kudokeza dhamira, kudokeza migogoro, kuonesha suluhisho la mgogoro, kutoa adili au funzo, kufikirisha hadhira na kuiachia hadhira hamu ya kusoma kazi nyingine za watoto. Kwa upande wa miisho dhima yake katika nathari za watoto za Kiswahili ni pamoja na kutoa majibu, kumpa msomaji uhuru wa kutoa tathmini, kuonesha hali ilivyo, kuonesha suluhisho, kutoa funzo/adili, kujenga taharuki, kushirikisha hadhira na kutoa majibu kwa maswali yaliyoulizwa. Kwa ujumla mianzo na miisho katika nathari za Kiswahili za watoto ni vipengele vya lazima katika kazi yoyote ya fasihi (taz. Adamo, 1995), vinahusiana na kutegemeana kwa kiasi kikubwa. Hii ni kusema kuwa hakuna kazi ya fasihi ambayo haina mwanzo na vivyo hivyo kazi hiyo ina mwisho. Aidha, vipengele hivi pamoja na vipengele vingine kwa pamoja huhusika katika kujenga muundo katika kazi ya nathari.

## Marejeleo

Adamo, G. (1995). "Beginnings and Endings in Novels." Katika *New Readings*. kur. 83-104.

Hood, D. (2012). "Writing Creative Nonfiction: Beginning and Ending" https://davehood59.wordpress.com/2012/08/16/writing-creative-nonfiction-beginning-and-ending iliyosomwa tarehe 22/06/2015.

Liu, Y. (2009). “Significance of Structure in Analyzing Short Stories.” Katika *Asian Social Science*. 5(5): 141-143.

Lyimo, E.B. (2014). “Usaguzi wa Kijinsia katika Vitabu vya Kiswahili vya Fasihi ya Watoto na Mtazamo wa Wadau nchini Tanzania.” Tasnifu ya Uzamivu (Haijachapishwa) Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.

Madumulla, J.S. (2009). *Riwaya ya Kiswahili: Nadharia, Historia na Misingi ya Uchambuzi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Ltd.

Mulokozi, M.M. (1996). *Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Chuo Kikuu Huria cha Tanzania.

Pattison, D. (2012). Endings v. Beginnings: Which is More Important? file:///F:/Endings%20v_%20Beginings%20Which%20is%20More%20Important%20%E2%80%94%20Fiction%20Notes.htm iliyosomwa tarehe 12/10/2015.

Senkoro, F. E. M. K. (2006). Fasihi ya Kiswahili ya Majaribio: Makutano baina ya Fasihi Simulizi na Fasihi Andishi. Katika *Kioo cha Lugha* Na 4. Dar es Salaam: TUKI. kur. 22-38.

Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Limited.

Wafula, R. M. na Njogu, K. (2007). *Nadharia za Uhakiki wa Fasihi*. Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Wamitila, K. W. (2002). *Uhakiki wa Fasihi: Misingi na Vipengele vyake.* Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Wamitila, K. W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide-Muwa Publishers Limited.

Wamitila, K.W. (2008). *Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Limited.

### Vitabu Teule

Abeid, M. (1996). *Mji wa Mawe II*. Dar es Salaam: M & K Publishers and Agencies Limited.

Abeid, M. (2003). *Mtego Kabambe*. Dar es Salaam: Mathews Bookstore and Stationers.

Byeyombo, H. H. (2003). *Polisi Kipofu*. Dar es Salaam: Tamba General Enterprises Ltd

Bwana, J. H. (2003). *Mganga Pazi*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited

Dumea, P.H. (2006). *Chifu Mahawanga*. Dar es Salaam: Readit Books Ltd.

Ebraju, P.B. (1999). *Sababu mimi ni Mwanamke!*. Dar es Salaam: Educational Books Publishers Ltd.

Lema, E. (1998). *Mwendo*. Dar es Salaam: E & D Limited.

Lema, E. (2001). *Ndoto ya Upendo*. Dar es Salaam: E&D Limited

Lingindo, R.M.K. (2000). *Wawindaji Watatu*. Dar es Salaam: Oxford University Press (T) Ltd

Lotto, M.M. (1999). *Laba Msichana Shujaa*. Dar es Salaam: HEKO Publishers Ltd.

Manji, A. (2006). *Wateka Nyara*. Dar es Salaam: Press and Publicity Centre Limited.

Mgeta, Kombe, Daffa & Chuwa (2005). *Chatu na Mbwa*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.

Mkufya, W.E. (2009). *Wema Amwokoa Noa*. Dar es Salaam: Mangrove Publishers.

Mnyaka, O. (2005). *Kimbia! Helena, Kimbia!* Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Mnyaka, O. (2007). *Cheka Kidogo, Helena!* Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Mnyaka, O. (2009). *Vipaji vya Helena*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.

Moshi, R. (1995). *Sinderela*. Dar es Salaam: Mture Educational Publishers Limited.

Moshi, S.E. (2003). *Kibo na Mawenzi*. Dar es Salaam: Mture Education Publishers Limited.

Mpembulles, N. (2008).*Urafiki wa Ngedere na Mamba*. Dar es Salaam: Kwanza Publishers Limited.

Mtobwa, B.R. (2000). *Mpishi Mwenye Kibiongo*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.
Mulokozi, M.M. (2006). *Ngome ya Mianzi*. Dar es Salaam: Sasa Sema Publications.
Mwandoloma, N. (1991). *Tanzua*. Arusha: Eastern Africa Publications Limited.
Mwenda, D. (1995). *Bahati na Mumewe*. Dar es Salaam: Educational Publishers and Distributors Ltd.
Mzindikaya, C. (2005). *Joka Lenye Vichwa Saba*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.
Paul, F. (2006). *Pete ya Bahati*. Dar es Salaam: Heko Publishers Ltd.
Sabuni, E.G. (2008). *Zindera*. Dar es Salaam: Solution Publishing.